




Mamlaka ya
Mawasiliano
Tanzania



Tanzania inavyojipanua Kidijitali

The Regulator

Aprili-Juni 2026

Jarida la kila Robo Mwaka
la Mamlaka ya Mawasiliano
Tanzania (TCRA)

ISSN: 0856 - 8030
4-2025/2026



INA ITHIBATI YA ISO 9001:2015 CERTIFIED www.tcra.go.tz

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania



Dira

Jamii iliyowezeshwa na huduma za mawasiliano jumuishi na endelevu



Dhima

Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa jamii ya Watanzania.



Wajibu

Wajibu wa Mamlaka ya Udhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni kusimamia sekta ya mawasiliano na kielektroni na posta kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania Namba 12 ya mwaka 2003.



Tunu Kuu

1. WELEDI



Tunatekeleza majukumu yetu kwa kutoa huduma bora bila upendeleo tukizingatia maadili na heshima stahiki kwa wadau wetu.

2. UBUNIFU



Tunazingatia ubunifu na kuendelea kuboresha na kushughulikia masuala ya usimamizi kwa kuzingatia yanayotokea kwenye mazingira ya teknolojia ambayo yanabadilika kila wakati.

3. UTENDAJI WA PAMOJA



Tunaamini katika nguvu ya ziada inayotokana na utendaji kazi wa pamoja na ushirikiano ili kufikia malengo ya pamoja, kwa kutambua kuwa mawasiliano kwa njia ya ufanisi na inayojenga ni muhimu ili kujenga mazingira yanayochangia ushirikiano kwenye shughuli zetu.

4. WEPESI KUBADILIKA



Tumejiandaa kubadilika, kuendana na mabadiliko na kukabiliana na kuendana na yanayojitokeza, teknolojia na changamoto za usimamizi kwenye sekta ya mawasiliano.

Anwani ya ofisi za uhariri.

Mawasiliano Towers Na. 20 Barabara ya

Sam Nujoma, S.L.P 474, Postikodi: 14414 Dar es Salaam. Simu: +255 784558270, +255 784558271. baruapepe: regulator.magazine@tcra.go.tz; dg@tcra.go.tz. Toleo la kidijiti linapatikana mtandaoni kwenye: <https://www.tcra.go.tz/documents/the-regulator>

Regulator linatolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania

Wajibu na kazi za TCRA kwa mujibu wa Sheria:

1. Kukuza ushindani bora na uchumi wenye tija.
2. Kulinda maslahi ya watumiaji.
3. Kulinda mitaji ya Watoa Huduma wenye ufanisi.
4. Kukuza upatikanaji wa huduma zinazosimamiwa kwa watumiaji wote wakiwamo wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji walio na walioko katika mazingira magumu.
5. Kuimarisha Elimu kwa Umma, uelewa na ufahamu wa huduma zinazosimamiwa na TCRA, ikiwa ni pamoja na:
 - i. Haki na wajibu wa watumiaji na watoa huduma zinazosimamiwa;
 - ii. Namna ya kuwasilisha malalamiko na migogoro na utaratibu wa utatuzi wake; na
 - iii. Kazi na majukumu ya Mamlaka kwa kuzingatia umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.

TCRA inaendeleza upatikanaji wa huduma zinazosimamiwa kupitia utaratibu wa leseni za huduma za mawasiliano. Inasimamia masharti ya leseni na ya kanuni zinazotokana

na Sheria zinazohusu mawasiliano. Mamlaka inatoa leseni za huduma za mawasiliano na pia kufuta inapobidi kwa kuzingatia ubora wa utoaji huduma za Mawasiliano, Posta na Utangazaji.

Vilevile inasimamia utendaji wa watoa huduma katika sekta, ikiwa ni pamoja na

- a. Kuweka na kusimamia viwango kwa watoa huduma
- b. Kudhibiti ubora wa utoaji na usambazaji wa huduma.
- c. Kushughulikia malalamiko na kusuluhisha migongano na migogoro ndani ya sekta.
- d. Kushirikiana na wasimamizi wa mawasiliano wa nchi nyingine ili kuandaa mikakati itakayosaidia kuboresha utoaji huduma nchini.
- e. Kutekeleza mikataba ya kimataifa katika sekta ya mawasiliano
- f. Kuiwakilisha Tanzania kwenye mashirika ya kimataifa ya mawasiliano.
- g. Kutekeleza majukumu mengine yatakayopangwa kwa mujibu wa sheria za nchi.

Bodi ya Uhariri

Mwenyekiti

Mha. Mwesigwa Felician

Katibu

Bw. Rolf Kibaja

Wajumbe

Bw Semu Mwakyanjala (Coordinator)

Bw. Philip Filikunjombe

Bw. Peter Lyimo

Bw. Abel John

Bw. Robin Ulikaye

Bw. Vitalia Kidabulo

Bw. Alpha Wawa

Mhariri Uzalishaji

Bw. Isaac Mruma

Msanifu

Bw. Jackson Mkufya

Barua ya Mhariri

Msukumo mpya kuelekea Mageuzi ya Kidijiti Jumuishi Tanzania

Tanzania inashuhudia ongezeko kubwa la upanuzi wa miundombinu ya kidijiti na matumizi ya huduma za kidijiti. Maendeleo haya yanachangia kuimarisha ujumuishi wa kidijitali katika maeneo mbalimbali ya jamii na kuongeza uelewa wa wananchi kuhusu matumizi ya teknolojia.

Mambo haya yamefafanuliwa kwenye vipaumbele vinane (8) vya Serikali kwa sekta ya mawasiliano katika mwaka wa fedha wa 2026/2027, ambavyo vimechambuliwa katika makala kuu ya toleo hili.

Vipaumbele hivyo vimeainishwa wakati Tanzania ikiendelea kutekeleza Mradi wa Kidijitali wa Tanzania na Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Kidijitali.

Shughuli zilizopangwa zinatokana na vipengele muhimu vya nguzo za kupanua maeneo ya nchi kidijitali. Zinaimarisha misingi ya ukuaji endelevu wa kidijitali wa Tanzania.

Shughuli hizi zinajumuisha upanuzi wa mitandao ya mawasiliano ya ardhini na satelaiti, Msukumo ni kutumia miundombinu ya

kidijitali kwa uchumi wa kidijitali.

Shughuli nyingine ni pamoja na kuimarisha mfumo wa sera kwa kufanya mapitio ya sera na kanuni, kukuza ujuzi muhimu wa kidijitali, na kupanua uelewa wa wananchi kuhusu teknolojia.

Matumizi ya teknolojia zinazoibuka na fursa zake pamoja na kuimarisha usalama wa mtandao ili kujenga uaminifu katika huduma za kidijitali pia ni miongoni mwa mambo yatakayofanyika 2026/2027.

Takwimu za sekta ya mawasiliano za robo ya mwisho wa mwaka wa fedha 2025/2025 (Aprili-Juni) zinaonyesha ongezeko kubwa la matumizi ya intaneti na data, hivyo kuimarisha zaidi nguzo za maeneo ya kidijitali.



STENZ CON



04

Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu



05

Tanzania inavyopanua Maeneo ya Kidijiti



08

Vipaumbele sekta ya Mawasiliano 2026/2027




11

Kuelekea Ustahimilivu wa Kidijitali Tanzania



13

Akili Unde kwa Mageuzi Kijamii



17

Takwimu za Robo Mwaka



Ujumbe wa Mkurugenzi Mkuu

Kuwezesha Mawasiliano Wakati Wote

Watanzania wanazidi kutegemea mifumo ya kidijitali inayopanuka kwa kasi nchini pamoja na huduma zinazotolewa kupitia mitandao ya mawasiliano. Miundombinu imara na ya kuaminika ya kidijitali ni muhimu kwa maendeleo ya sekta zote kwenye uchumi wa nchi. Mfumo wa usimamizi Tanzania, ikiwa ni pamoja na utoaji leseni, unakuza ushindani, uvumbuzi, na uwekezaji katika sekta nzima.

Miundombinu inayoendelea kujengwa na kutumika nchini imepanua upatikanaji na wigo wa huduma za mawasiliano na kuongeza ujumuishi wa kidijitali. Pia imepanua fursa za wananchi kushiriki katika uchumi wa taifa.

Kati ya Machi 2021 na Juni 2026, asilimia ya watu wanaofikiwa simu za mkononi uzao wa tatu (3G) imeongezeka kutoka 70.3 hadi 93.95. Asilimia 94.39 wanafikiwa na uzao wa nne (4G), kutoka asilimia 50.4 mwaka 2021. Uzao wa tano (5G) umefikia asilimia 34.18 ya watu.

Kulikuwa na laini za simu zilizokuwa hewani 116,952,295, laini 62,793,986 zilizotumia intaneti na akaunti 87,046,089 za pesa kwa simu kufikia Juni 2026. Watumiaji wa huduma za pesa mtandaoni walifanya miamala 710,993,717. Simu janja zimeenea kwa asilimia 44.7 ya watu.

Uchumi wa Tanzania, huduma za umma, na mifumo ya kitaifa sasa inategemea mitandao ambayo lazima ifanye kazi katika hali ya kawaida na wakati wa matatizo na changamoto mbalimbali ikiwemo kukatika. Kukatika kwa mawasiliano kuna athari kubwa kwa mitandao, kwa watumiaji na kwa uchumi wa nchi.

Utekelezaji wa mipango inayohakikisha ustahimilivu wa kidijitali unavuka mipaka ya kitaifa. Katika ulimwengu wa leo

uliunganishwa, hakuna nchi inayofanya kazi peke yake.

Nyaya za faiba za kimataifa zinazopita chini ya bahari, mifumo ya setilaiti, mitandao ya nyaya za faiba zinazovuka mipaka nchi kavu, na mtiririko wa data duniani unafungamanisha uchumi na jamii zetu. Matukio yanayofuatana ya usumbufu na kuvurugika au kukatika sehemu moja ya mitandao vinaweza kuwa na athari kubwa katika maeneo mengine.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika kupanua ueneaji wa mifumo ya mawasiliano kidijitali ili kuhakikisha kuwepo mitandao na huduma vinavyotegemewa na endelevu. Nchi imepata maendeleo makubwa katika kuimarisha ustahimilivu wa miundombinu yake ya kidijitali.

Vilevile Tanzania imeimarisha ustahimilivu wa mitandao ambayo imeunganaishwa ndani ya nchi, kikanda na kimataifa kupitia Mkongo wa Kitaifa wa mawasiliano ya kasi (NICTBB) na nyaya nne za faiba za kimataifa zilizoingia nchini kupitia baharini. Kuna vituo sita vya kuwezesha mawasiliano ya intaneti na vituo vinne vya data vinavyotumiwa na watoa huduma wote ili kufanikisha huduma za mawasiliano nchini.

Hizi zinahakikisha kuwa kunakuwa na njia mbadala za kupitisha mawasiliano na hivyo kupunguza hatari ya sehemu moja ya mitandao kushindwa kufikisha huduma. Zinapunguza ucheleweshaji na kuhakikisha mwendelezo wa huduma hata wakati wa kukatika, kuvurugika au usumbufu kimataifa.

Tumeshughulikia ustahimilivu katika mzunguko mzima na hatua zote za mifumo ya kidijitali - kuanzia usanifu, uendeshaji na urejeshaji wa huduma zinapokatika. Mifumo yetu ya usimamizi inajumuisha urejeshaji, uelekezaji

mawasiliano kwenye njia mbadala, usalama wa mtandao, na uchangiaji wa miundombinu.

TCRA inawataka waendeshaji kujenga mitandao thabiti na stahimilivu kupitia urejeshaji na njia mbadala, utayari wa usalama wa mtandao, ushirikiano, na mifumo bora ya urejeshaji yenye ufanisi, na kudumisha huduma muhimu kwa wakati uleule zinapohitajika.

Kupitia ufuatiliaji na uratibu ulioimarishwa, watoa huduma wako katika nafasi nzuri ya kugundua hitilafu mapema, kupanga upya njia za kupitisha mawasiliano kwa ufanisi, na kudumisha huduma muhimu kwa wakati uleule zinapohitajika.

Tunaendelea kuimarisha uwezo wa kitaasisi, ikiwa ni pamoja na Kitengo cha Kitaifa cha Kushughulikia Masuala ya Dharura ya Usalama wa Mitandao (TZ-CERT), ili kuhakikisha mwitikio wa haraka, usimamizi mzuri wa matukio, na uboreshaji endelevu wa usalama wa mitandao.

Vilevile tunakamilisha Mfumo wa Usimamizi wa Migogoro (CMF) wa sekta nzima ambao utaongeza utayari, uratibu, na mwendelezo wakati wa dharura za mawasiliano. Mfumo huu utasaidia mwitikio kwa wakati unaofaa na kuimarisha uwezo wa sekta hii wa kudumisha huduma muhimu za mawasiliano wakati wa migogoro, kuvurugika na usumbufu mwingine.

Ustahimilivu wa kidijitali ni jukumu la pamoja. Unahitajika ushirikiano endelevu miongoni mwa wasimamizi, kampuni za mawasiliano, watoa huduma za teknolojia, na washirika wa kimataifa, ukiwa unaongozwa na mifumo na ushirikiano wa kimataifa kupitia taasisi za kikanda na kimataifa.

Tanzania inavyopanua maeneo ya Kidijiti Na Mwandishi wa Regulator

Azma ya Tanzania kupanua kwa kiasi kikubwa maeneo ya teknolojia za kidijiti imetafsiriwa kwenye maeneo manane (8) ya kimkakati ambayo Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imejizatiti kuchangia kuyawezesha.

Maeneo hayo, yaliyowasilishwa Bungeni hivi karibuni yanahusisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano, kuendeleza

(TEHAMA), kuimarisha ulinzi mitandaoni na kuweka mazingira wezeshi yatakayochosha ubunifu na kupanua uelewa wa wananchi.

Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angela Kairuki amesisitiza kuwa Tanzania imepanga kujenga jamii iliyounganishwa na jumuishi kidijiti ifikapo 2050.

Kuelekea ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

Amefafanua kuwa mkakati huu unalenga kufikia malengo ya Dira ya Taifa 2050 ambayo inasisitiza umuhimu wa teknolojia za kidijiti kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii.

Dira hiyo, iliyoanza kutekelezwa mwaka huu, inalenga kuifanya Tanzania kuwa kitovu cha TEHAMA ukanda huu wa Afrika na Barani.

Mipango kabambe itatekelezwa kueneza miundombinu ya mawasiliano ya kidijiti na kuwezesha uunganishaji wa watu zaidi. Huduma za TEHAMA zitaendelezewa kama zilivyo nyingine za msingi kama maji na nishati.

Maeneo ya mipaka ya kidijiti ya nchi ni mipango endelevu ya nchi kujenga na kuimarisha teknolojia mpya ambazo zinaleta uwezekano mwingi kwa jamii.




Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhe. Angella Kairuki, akipokea tuzo kutoka Umoja wa Kimataifa wa Mawasiliano (ITU) kwa kutambua jitihada za Tanzania za kuendeleza maendeleo endelevu kupitia mawasiliano ya kidijitali, hususan ujenzi wa minara 758 mipya ya mawasiliano ya simu.

Nguzo Muhimu

Mipaka hii inapanuliwa kwa kuzingatia nguzo kadhaa. Tanzania imefanikiwa kuimarisha nguzo zinazoweza ukuaji wa sekta kwa kutekeleza sera na mikakati inayohimiza ushirikiano wa sekta mbalimbali.

Nguzo hizi ni pamoja na miundombinu ya kidijiti, uimara na ustahilivu wake na upatikanaji wa huduma kupitia miundombinu hii. Nyingine ni namna teknolojia za kidijiti zinavyochukuliwa kwa matumizi kutokana na umuhimu wake kwenye maisha na shughuli za watu na taasisi.



Matumizi ya huduma na bidhaa wezeshi za mawasiliano yanajenga mwelekeo ambao unachangia kukua kwa maeneo mengi ya kiuchumi, kijamii na kiutawala. Hii inatokana na mawasiliano kuwa sekta wezeshi.

Matumizi ya huduma na bidhaa wezeshi za mawasiliano yanajenga mwelekeo ambao unachangia kukua kwa maeneo mengi ya kiuchumi, kijamii na kiutawala. Hii inatokana na mawasiliano kuwa sekta wezeshi.

Mabadiliko na kukua kwa sekta kunachangiwa na wahusika wengi kuanzia msimamizi, watoa huduma na taasisi nyingine kwenye mfumo wa utoaji huduma za kidijiti.

	Aprili	Mei	Juni
Airtel Money	14,164,833	14,331,645	14,307,193
Azam Pesa	81,829	106,957	89,711
HaloPesa	7,932,463	8,473,702	8,796,709
Mixx by Yas	25,928,787	26,882,220	27,853,189
T-pesa	596,453	631,098	686,101
Mpesa	32,840,183	34,394,537	35,313,186
Jumla	81,544,548	84,820,159	87,046,089

Akaunti za Pesa kwa Simu kwa kila Mtoa huduma

Pamoja na mchango wa TCRA ambaye ni msimamizi wa sekta, wadau wengine pia wamechangia ukuaji huu na mabadiliko yanayoonekana.

Kwa mfano, serikali imepunguza gharama za kupitisha miundombinu kwenye hifadhi ya barabara. Ada hizi zinasimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA).

Kupatikana umeme vijijini kupitia miradi inayosimamiwa na Wakala wa Umeme Vijijini (REA) kumepunguza matatizo ya nishati maeneo mengi Tanzania.

Umeme wa uhakika unawezesha watumiaji kutumia vifaa vya kisasa zaidi kiteknolojia. Hii ni pamoja na kuweza kuchaji simu, kutumia ving'amuzi vya televisheni na vifaa vingine vya TEHAMA. Tanzania inajenga uchumi wa kidijiti na wa buluu, ambao mojawapo ya viwezeshi vyake ni mfumo imara wa malipo. Maendeleo ya sekta yamawezesha ujumuishi wa huduma za kifedha kidijitali.

Ukuaji pesa mtandaoni unaonesha mwelekeo huduma kwa wote. Zaidi ya asilimia 72 ya laini za simu za mkononi zinazotumika zina akaunti za huduma za pesa kwa njia ya simu, huku miamala ikiongezeka kwa asilimia 76 ndani ya miaka mitatu.

Huduma za fedha kwa njia ya simu Tanzania zinasimamiwa na TCRA, ambayo inatoa leseni kwa waendeshaji wa mitandao ya simu na kuwapa namba za mawasiliano na misimbo fupi inayotumika katika miamala na Benki Kuu ya Tanzania, ambayo inasimamia sekta ya huduma za kifedha nchini. Taasisi hizo mbili zinashirikiana katika masuala kadhaa.



Kiasi cha data kilichotumika kwa huduma za intaneti kila mwaka kati ya 2021 na 2026

Nguzo nyingine inayoweza kupanua maeneo ya kidijiti ni mfumo wezeshi wa kisheria na usimamizi/udhibiti. Huu unawezesha kuwepo watoa huduma wengi zaidi kupitia leseni, uanuai wa huduma, ubora wake na unafuu pia. Leseni zinaongeza ueneaji huduma na matumizi.

Ongezeko Leseni

Kufikia Juni 2026, TCRA ilikuwa imetoa leseni 53 za mitandao ya mawasiliano (NF), 26 za huduma za mtandao (NS) na 180 za huduma tumizi za mawasiliano (AS).

Leseni za NF Leseni hizi zinamruhusu mtoa huduma kumiliki miundombinu kama minara ya mawasiliano ya simu za mkononi, minara na vifaa vya kurushia matangazo ya vyombo vya utangazaji na nyaya za simu na mitambo ya mawasiliano.

Leseni za NS zinamruhusu mwenye leseni kutoa huduma za msingi za kuunganisha mitandao mbalimbali ya mawasiliano. Hizi ziliongezeka kutoka 25 hadi 26. Ingawaje mwenye leseni hii pia anaweza kuwa na leseni ya miundombinu, mfumo wa leseni unaruhusu watoa huduma kutumia miundombinu ya wengine.

Ueneaji huduma

Tanzania imefanikiwa kufanya haya yote na kuweka misingi ya kuyaendeleza. Serikali imetekeleza miradi ya kuboresha miundombinu kwa kuweka teknolojia za kisasa na zinazowesha huduma bora zaidi na kufika na kupatikana maeneo mengi nchini.

Takwimu za sekta ya mawasiliano kufikia Juni 2026 zinaonesha kuwa teknolojia za mawasiliano uzao wa tatu (3G) zimeenea kwa asilimia 93.95 ya watu na uzao nne (4G) asilimia 94.39.

Usambazaji na uwekaji wa miundombinu ya teknolojia ya mawasiliano ya simu uzao wa tano (5G) unaongezeka kwa kasi tangu ilipoingia nchini 2022. Kufikia Juni ulifikia asilimia 34.18 ya watu, hali inayoonesha ukuaji wa kasi.

Utangazaji na Posta

Pamoja na uimarishaji wa miundombinu ya huduma za TEHAMA, huduma za utangazaji na posta pia zimeboreshwa. Ofisi nyingi za posta mijini zimefanywa vituo vya huduma za jamii zinazopatikana sehemu moja.

Miundombinu ya posta ni pamoja na mfumo wa anwani za makazi na postikodi. Huu unatarajiwa kufanikisha biashara mtandao, kwani bidhaa zinazonunuliwa kupitia miamala ya kidijiti zinachukuliwa au kufikishwa kwa watu pale walipo.

Tanzania, ikiwa imezungukwa na nchi nane, ambao tano hazina mwambao wa bahari iko kwenye nafasi kubwa kimbakati kuvuna matunda ya biashara mtandao moja kwa moja au kutokana na shughuli kwenye mlolongo wa utoaji huduma za kiposta.

Unafuu wa gharama

Kushuka kwa gharama za mawasiliano na unafuu wa upatikanaji na matumizi vimepanua matumizi na watumiaji. Gharama za simu za maongezi zimeshuka mara sita kati ya Juni 2021 and Juni 2026.

Gharama ndani za simu ndani ya mtandao zimeshuka kutoka shilingi 149 hadi 28 kwa dakika, huku gharama nje ya mtandao zikitoka shilingi 189 hadi 28. Kuwepo kwa gharama sawa ndani na nje ya mtandao kumeleta ufanisi kwenye mawasiliano na unafuu kwa mtumiaji.

Usalama Mitandaoni

Uimarishaji wa usalama mitandaoni umejenga imani ya watumiaji kwenye huduma za kidijiti. Mikakati ya kuhakikisha usalama ni pamoja na kufuatilia kanuni na kukabiliana na viashiria vya uhalifu mitandaoni.

TCRA na Uvumbuzi

Ubunifu na uvumbuzi kwenye sekta pia vimechangia ueneaji wa huduma. Sera ya Taifa ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), ambayo imepitwa upya na kurekebishwa, inatambua mchango wa mazingira wezeshi ya kisera na kiusimamizi kwenye kukuza uvumbuzi kidijiti.

Sera hiyo inalenga kuibadili Tanzania kuwa ya kidijiti, yenye uchumi imara ambao unawezesha na kuendeleza uvumbuzi na ujasiriamali wa kidijiti. Vilevile lengo ni kuwezesha Tanzania kufikia na kupita malengo ya kikanda Afrika na kimataifa kama yalivyoainishwa kwenye Ajenda ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu ifikapo 2030 na yale ya Dira ya Umoja wa Afrika 2063.

Mipango itatekelezwa kuendeleza miundombinui ya TEHAMA na kuwekeza kwenye huduma za kidijiti zenye ubunifu.

Mifumo ya Kisheria/Kikanuni, kulingana na muktadha

TCRA inaendelea kutekeleza wajibu wake muhimu wa kusimamia sekta ya mawasiliano nchini Tanzania. Inaweka mazingira wezeshi ya kikanuni, inaendesha programu zinazolenga ushirikishwaji wa wote, na kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kuwa wananchi na taifa kwa ujumla wananufaika na mapinduzi ya kidijitali.

TCRA inachangia katika uchumi wa kidijitali na uchumi wa buluu kupitia majukumu yake ya usimamizi, ikiwa ni pamoja na utoaji wa leseni, ufuatiliaji wa utendaji na uzingatiaji

wa masharti, pamoja na utekelezaji wa kanuni. Mamlaka inahamasisha upatikanaji wa muunganisho na huduma bora kwa kiwango kinachofaa.

Mapitio ya Kanuni za Utoaji wa Leseni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta ya mwaka 2022, yaliyoanzishwa na TCRA, yamefungua fursa mpya kwa wajasiriamali katika sekta ndogo za utangazaji na posta. Kanuni hizo zimeanzisha aina ndogo mbalimbali za leseni chini ya aina kuu nne za leseni katika mfumo jumuishi wa utoaji wa leseni za mawasiliano, pamoja na kuweka masharti ya utoaji wa leseni za biashara mtandao.

Mikakati yalenga Miundombinu, Biashara Mtandao, Ujasiriamali

Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari imeanisha Maeneo yapatayo 30 chini ya Vipaumbele vinane Mwaka wa Fedha 2026/2027

1 Kutunga, kuhuisha na kusimamia utekelezaji wa Miongozo inayosimamia Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari (TEHAMA).

Yatakayofanyika:

- i. Kusimamia utekelezaji wa Mikakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Mwaka 2024 – 2034.
- ii. Kukamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Posta ya Mwaka 2003 Toleo la Mwaka 2026.
- iii. Kukamilisha utungwaji wa Sera Mpya ya Taifa ya TEHAMA ya Mwaka 2026.
- iv. Kukamilisha utungwaji wa Sera ya Taifa ya Anga za Juu na Sera ya Taifa ya Kampuni Changa ya Mwaka 2026.
- v. Kukamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mkataba wa Umoja wa Afrika wa Usalama wa Mtandao na Ulinzi wa Taarifa Binafsi wa Mwaka 2014.
- vi. Kukamilisha taratibu za uridhiwaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Uhalifu wa Mtandao wa Mwaka 2025 na Mikataba miwili ya Kimataifa ya Anga za Juu.
- vii. Kuendelea na taratibu za utungwaji wa Sheria ya Anwani za Makazi ya Mwaka 2026 na Sheria ya TEHAMA ya Mwaka 2026..

Vipaumbele Sekta ya Mawasiliano 2026/2027

2 Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Posta

- Kuimarisha upatikanaji wa Huduma za Mawasiliano ya Simu na Redio katika maeneo yasiyo na mvuto kibishara.
- Kukamilisha ujenzi wa Minara 636 katika Kata 443 zenye Vijiji 636 na kuendelea na ujenzi wa Minara 287.
- Kujenga Minara 280 katika maeneo ya Kimkakati yenye changamoto ya Mawasiliano kwenye Miundombinu ya Reli (SGR/MGR/TAZARA), Hifadhi za Taifa na Mipaka ya Nchi.

3 Kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kukuza na kuimarisha Biashara Mtandao

- Kuratibu na kusimamia Mradi wa Ujenzi wa Maghala ya Kuhifadhi Bidhaa za Biashara Mtandao.
- Kusimamia uundaji wa Mfumo wa Kidijitali utakaowezesha Biashara Mtandao.
- Kufanya tathmini ya Mifumo ya Kidijitali na usajili wa majukwaa ya Biashara Mtandao na Huduma za Kielektroniki.

4 Kuimarisha Miundombinu itakayowezesha utekelezaji wa Uchumi wa Kidijitali

- Kuunganisha Wilaya 10 na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.
- Kuunganisha Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika.
- Kuwezesha ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data Dodoma na Zanzibar.
- Kuwezesha usakinishaji na uboreshaji wa vifaa vya mikutano ya video katika Wilaya 100.
- Kuwezesha ufikishwaji wa huduma ya Wi-Fi katika maeneo 100 ya Umma.
- Kuratibu maunganisho ya Brodibendi kwenye Taasisi 100 za Umma, Mji wa Serikali Mtumba na Shule 100 za Umma; na Kuwezesha maunganisho 321,000 ya Miundombinu ya Huduma za Faiba.

5 Kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Anga ya Mtandao

- Kujenga uelewa kwa wananchi kuhusu ulinzi wa taarifa na Faragha zao na jinsi ya kukabiliana na matukio ya utapeli na wizi mtandaoni.
- Kuwezesha upatikanaji wa Mfumo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji wa Matukio na Makosa ya Mtandao.
- Kutoa elimu juu ya Miongozo ya Miundombinu Muhimu ya TEHAMA na kuimarisha Ulinzi wa miundombinu hiyo; Kuanzisha Kamati ya Kitaifa ya Usalama wa Mtandao.
- Kuandaa Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa Mkakati wa Usalama Mtandao.

6

Kuendeleza kampuni changa za TEHAMA (ICT Startups)

- i. Kusimamia uanzishwaji wa Taasisi ya Taifa ya Teknolojia ya Kidijitali – NDTI itakayojengwa Nala – Dodoma.
- ii. Kuwezesha uanzishwaji wa vituo saba (7) vya kukuza bunifu za TEHAMA.
- iii. Kufanya Tafiti tatu (3) za Matumizi ya Teknolojia za Kidijitali zinazoibukia katika Sekta za Uzalishaji na Huduma.
- iv. Kusimamia utekelezaji wa programu mbili (2) za uwezesaji wa wabunifu na Kampuni Changa za TEHAMA.
- v. Kuwezesha uanzishwaji wa vituo viwili (2) vinavyotembea vya kupata taarifa za TEHAMA (Mobile Information Access Centers).
- vi. Kusajili Kampuni Changa 100 za Ubunifu za TEHAMA.
- vii. Kuwezesha mafunzo kwa Kampuni Changa 25 za TEHAMA.

7

Kuimarisha Uwekezaji katika TEHAMA na utekelezaji wa Programu ya Anga za Juu

- i. Kuwezesha urushaji wa Satelaiti moja (1) katika Anga za Juu.
- ii. Kuratibu mradi wa kurusha Satelaiti ndogo ya mafunzo – CUBESAT.
- iii. Kujenga uelewa kwa Wananchi kuhusu matumizi ya Teknolojia ya Anga za Juu.

8

Kutoa Elimu kwa Umma kuhusu masuala yanayohusu TEHAMA na Teknolojia zinazoibukia

Kuelimisha Umma kupitia vyombo vya Habari na Mitandao ya Kijamii kuhusu matumizi sahihi na salama ya mawasiliano na kuwajengea uelewa wananchi kuhusu teknolojia zinazoibukia ikiwemo Akili Unde.



MITAZAMO

Kuelekea Ustahimilivu wa Kidijitali Tanzania

Na Mhe. Angela Jasmine Mbelwa Kairuki, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Hizi ni dondoo kutoka kwa ujumbe wa Mhe. Waziri kuhusu Siku ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Duniani (WCISTD) mnamo tarehe 17 Mei 2026. Mada ya mwaka huu ilikuwa "Tegemeo kuu maisha kidijiti: Kuimarisha Ustahimilivu katika Ulimwengu Uliunganishwa."

Kaulimbiu ya Siku ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Duniani ya mwaka huu (WCISTD) imekuja kwa wakati unaofaa kutukumbusha kwamba muunganisho wa kidijiti si anasa tena; ni miundombinu muhimu ya kitaifa.

Hapa Tanzania, majukwaa ya huduma za pesa kupitia simu za mkononi yanahusisha miamala ya mabilioni ya shilingi kila siku. Huduma za dharura hutegemea mawasiliano ya simu ya kuaminika na yanayowezeshwa kuwa na kasi na mawitiko wa haraka. Huduma muhimu za umma za afya, elimu, na fedha zinazidi kuimarishwa na mitandao ya kidijiti inayojumuisha miundombinu ya simu za mkononi na mezani, nyaya za faiba, setilaiti, na vituo vya data.

Hata hivyo, migogoro iwe inayoonekana na, inayohusiana na mtandao, ya asili, au ya bandia — inaweza kuvuruga huduma hizi, na kuathiri usalama wa umma, maisha ya watu, utulivu wa kiuchumi, na usalama wa taifa.

Tanzania imepiga hatua kubwa katika mawasiliano ya intanei ya kasi. Hata hivyo, kupanua maeneo yaliyounganishwa pekee hakutoshi. Lazima pia tujenge mifumo ya kidijitali imara — mifumo ambayo inaweza kuhimili mshtuko, kubadilika kuweza kufanya kazi kwenye mazingira yaliyopitita misukosuko, na kurudia hali ya kawaida haraka.

Uzoefu wa hivi karibuni kimataifa, ikiwa ni pamoja na matukio ya hali mbaya ya hewa na kukosekana huduma kutokana na kasoro kwenye miundombinu mikubwa, umeonyesha jinsi mitandao ya kidijiti inavyoweza kuwa dhaifu pale ambapo ustahimilivu haukujengwa kuanzia hatua za awali.

Ustahimilivu lazima uwekwe kikamilifu ndani ya mfumo mzima wa kidijiti. Hii ina maana kubuni mifumo inayowezesha huduma kutolewa kwa njia na mfumo tofauti, utayari wa usalama wa mtandao, ushirikiano usio na ukomo, na miundombinu endelevu.

Inamaanisha kuwa na uwezo wa kukabiliana haraka kubadilisha njia za mtandao na mawasiliano ya dharura yenye ufanisi wakati wa maafa. Na ina maana ya kuwekeza katika urejeshaji wa huduma haraka na kuimarisha mfumo ili kulinda miundombinu dhidi ya usumbufu wa siku zijazo.

Kutafuta ustahimilivu wa kidijiti kwa Tanzania kunategemea Dira ya Maendeleo ya Tanzania ya 2050, ambayo inatambua mabadiliko ya kidijitali kama kichocheo cha matarajio ya muda mrefu ya kijamii na kiuchumi ya nchi. Kufikia maono haya kunahitajika miundombinu imara, salama, na thabiti ya kidijitali inayowezesha maendeleo jumuishi na endelevu katika sekta zote.

Mfumo wa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Tanzania (2024–2034) unaimarisha zaidi azma hii kwa kuainisha hatua madhubuti za kulinda miundombinu muhimu ya kitaifa ya mawasiliano kidijitali, data, na rasimali nyinginezo. Hizi ni pamoja na ukuzaji na uendeshaji wa Miongozo ya Kitaifa ya Miundombinu Muhimu ya teknolojia za kidijiti (CII), Miundombinu Muhimu ya Kitaifa ya Umma (NPKI), na mifumo ya kujikinga dhidi ya vitisho vinavyoibuka vinavyoonekana na vya kimtandao.

Jukumu la Tanzania kama kitovu cha kuunganisha mawasiliano kikanda linasisitiza umuhimu wa njia za kidijitali zinazostahimili. Kufikia Desemba 2025, Mkongo wa Kitaifa wa Mawasiliano ya kasi (NICTBB) ulikuwa na urefu wa kilomita 15,167 na uwezo wa Gbps 2,000. Uliunganisha makao makuu yote ya mikoa Tanzania Bara, wilaya 122 kati ya 139, na nchi saba jirani.

Kazi inaendelea kuunganisha wilaya zilizobaki na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.

Kufikia Machi 2026, Tanzania ilikuwa na nyaya nne ya faiba zinazopita baharini zilizotua Dar es Salaam. Aidha kulikuwa na vituo sita vya intaneti kimataifa (IXPs), na vituo vitano vya data vilivyoidhinishwa kuhifadhi mifumo muhimu ya shughuli za nchi.

Uimarishaji wa njia hizi za kuokoa maisha kunahakikisha mwendelezo wa huduma, biashara, mawasiliano ya dharura, na uchumi wa kidijitali katika eneo lote hata wakati wa matukio ya mtandaoni, majanga ya asili, au kushindwa kwa miundombinu.

Tanzania imeanzisha mfumo imara wa kisheria na kitaasisi wa kujiandaa na kukabiliana na majanga na dharura. Sheria ya Usimamizi wa Maafa Namba 7 ya 2015 ilianzisha Wakala wa Usimamizi wa Maafa Tanzania (TDMA), ambao hutoa mfumo wa kitaifa wa usimamizi wa hatari ya majanga na kuwezesha mipango ya dharura mahususi ya sekta.

Katika mawasiliano ya simu, Mpango wa Kitaifa wa Mawasiliano ya Dharura (NETP) unaongoza utayari na njia za kushughulikia maafa. Unaweka lengo la kurejesha huduma za mawasiliano ndani ya saa 24 baada ya janga. Unasisitiza tathmini ya hatari, mafunzo, na mazoezi ya kujiandaa ili kuimarisha utayari wa kitaifa.

Mkakati wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) wa Usimamizi wa Masafa wa 2024/25–2034/35 unatambua zaidi mawasiliano ya dharura kama kazi muhimu ya kitaifa.

Usalama wa mtandao unabaki kuwa nguzo muhimu ya ustahimilivu wa kidijitali. Kupitia TCRA, Tanzania imeanzisha Kitengo cha Kukabiliana na Dharura za Kompyuta Tanzania (TZ-CERT) chini ya Sheria ya

Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta, 2010. TZ-CERT hufuatilia, hugundua na hukabiliana na vitisho vya usalama wa mtandao ili kulinda miundombinu muhimu ya kidijitali ya nchi na kuhakikisha mawasiliano salama na yasiyokatizwa.

Jitihada hizi za pamoja zimeimarisha kwa kiasi kikubwa ustahimilivu wa Tanzania kidijitali. Aidha umechangia kuwezesha Tanzania kufikia Daraja la Kwanza la "Mfano wa Kuigwa" katika Faharasa ya Usalama wa Mtandao Duniani (GCI) mwaka 2024.

Kujenga ustahimilivu wa kidijitali hakuwezi kupatikana kwa kutengwa. Mifumo ikolojia ya kidijitali huvuka mipaka ya kitaifa na hivyo hukabiliwa na usumbufu ambao unaweza kuathiri nchi nyingi kwa wakati mmoja.

Kupitia ushirikiano na Shirika la Mawasiliano Ulimwenguni (ITU) na mashirika ya kikanda, Tanzania inaendelea kuhakikisha kuwa mtandao yake ni imara, salama, na jumuiishi.

Tunapoadhimisha siku hii muhimu, tunapata fursa ya kutafakari kuhusu tegemeo la maisha kidijitali lisiloonekana na linaloweza uchi wetu kuendelea na watu wetu kushikamana. Tuweke upya ahadi yetu ya kuimarisha tegemeo hili ili kukabiliana na changamoto zilizo mbele yetu.

Kwa pamoja, tunaweza kujenga mustakabali wa kidijitali ulio imara, jumuiishi, na kwa wote.



Mhe. Angellah Jasmine Mbelwa Kairuki, Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, akikabidhi zawadi ya kumbukumbu wakati wa ziara yake Viettel Group, Hanoi, Vietnam. Waziri Kairuki ameitaka Viettel kuendelea kuwekeza Tanzania, hususan katika kupanua mtandao wa Halotel 4G na 5G



Akili Unde kwa Mabadiliko ya Kijamii

Na Mwandishi wa Regulator

Wataalamu wa teknolojia na uchumi wametoa wito wa kuweka mfumo wa kisheria na kiudhibiti wa matumizi ya uwezo wa akili unde (AI) kubadilisha jamii na kuhamasisha uwajibikaji kwenye utoaji wa maudhui.

Mkutano wa hivi karibuni wa wadau kuhusu maadili ya AI na udhibiti wa mabadiliko ya kijamii uliainisha njia za kushughulikia changamoto changamani za kijamii zinazosababishwa na teknolojia zinazoibuka. Lengo ni kuhifadhi maadili ya jamii na kukuza maelewano.

AI ni nadharia ya kuunda mifumo ya kompyuta yenye uwezo wa kufanya kazi zinazohitaji akili ya binadamu, kama vile kuona, kutambua sauti, au kutafsiri lugha.

Mkutano huo, ulioitishwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO), ulibainisha kuwa faida na fursa za mabadiliko ya teknolojia ya kidijitali na fursa zake hazipaswi kufifishwa na changamoto zinazoweza kutatuliwa kwa urahisi.



Changamoto hizo ni pamoja na usumbufu wa kijamii, ukosefu wa usawa na taharuki na wasiwasi wa kimaadili unaoweza kusababishwa na AI. Nyingine ni habari potofu kupitia usambazaji wa picha na video zinazozalishwa na AI. Haya yanaleta hofu miongoni mwa umma.

Maudhui kutoka nje ya nchi yanaweza pia kukinzana na maadili ya kitamaduni, kanuni za kijamii na hali halisi za lugha. Matumizi ya kina ya AI na utegemezi pia husababisha baadhi ya kazi kutoweka kutokana na mambo kufanyika kiotomatiki, kwa kupunguza uingilaji wa kibinadamu katika kazi nyingi.



Hii inaleta mahitaji ya kuimarisha utafiti na utekelezaji wa sera unaotegemea ushahidi ili kuwezesha mabadiliko chanya ya kijamii na matokeo ya maendeleo endelevu.



UNESCO inazihimiza nchi wanachama kuhakikisha kwamba maendeleo, kupatikana na matumizi ya AI vinaleta athari chanya za kijamii na kuzingatia haki za binadamu, utu na maendeleo endelevu.

Serikali zinapaswa kukuza uvumbuzi wa ndani ili kuhakikisha matokeo chanya ya kijamii katika enzi ya AI.

Wanapaswa kuunda mazingira wezeshi ambayo yanasaidia vijana na wabunifu kubadilisha mawazo yanayohusiana na muktadha kuwa biashara zinazokua.

Hii ni pamoja na kuimarisha biashara na kuwezesha upatikanaji wa uwekezaji na masoko.

Mipango hii pia inapaswa kuzingatia matumizi ya AI kwa njia inayohakikisha kuwajibika na ya kimaadili. Lengo linapaswa kuwa kuwapa watu ujuzi na uelewa wa teknolojia ya AI, fursa zao, hatari, na matumizi sahihi.

Ubia wa Sekta ya Umma na Kibinafsi (PPPs) unapaswa kutumika ili kukuza miundombinu ya kitaifa ya AI ili kuchochea uvumbuzi na kuondoa tofauti za matumizi na huduma na vifaa vya kidijitali.

Miundombinu hii inapaswa kujumuisha vifaa vinavyoweza utendaji wa mifumo ya kompyuta yenye ufanisi wa juu (kama vile kuhifadhi data mitandaoni na kwenye vituo vya data) na miundombinu ya mfumo ikolojia wa data.

Nchi zinapaswa pia kukuza ufahamu na ujuzi wa kidijitali miongoni mwa watu wao ili kuwawezesha kutofautisha kati ya maudhui halisi na yanayotokana na AI.

Wakati huo huo, Tanzania itakuwa mwenyeji wa Kongamano la Afrika la Mabadiliko ya Kijamii na Maadili ya AI Agosti mwaka huu.

Watafiti, watunga sera, na wabunifu kutoka kote barani Afrika wataweza kuonesha utafiti, kushiriki mbinu bora, na kujadili jinsi AI inaweza kuendesha mageuzi ya kuwajibika kijamii na kiutamaduni.

Mapendekezo ya UNESCO kuhusu AI

Yamejikita kwenye msingi wa kanuni kumi:

Uwiano na kuondoa madhara

Mifumo ya AI inapaswa kuundwa na kutumiwa kwa njia zinazoepusha madhara na kuhakikisha kuwa hatari zinalingana.

Usalama na Ulinzi

Mifumo ya AI lazima iwe salama, imara, na thabiti na inayokabili misukosuko katika muda wote wa matumizi na iwe na njia za kuzuia matumizi mabaya, kuharibika (malfunction), au matokeo yasiyotarajiwa.

Usawa na Kutobagua

AI inapaswa kukuza usawa na kuepuka upendeleo, ubaguzi, na athari zisizo za haki kwa watu binafsi au vikundi.

Uendelevu

Ukuzaji wa AI na matumizi yake vinapaswa kusaidia uendelevu wa mazingira, ustawi wa jamii, uchumi na maendeleo ya muda mrefu.

Haki ya Faragha na Ulinzi wa Data

Mifumo ya AI lazima iheshimu haki za faragha na kuhakikisha usimamizi thabiti wa data, uwazi na ulinzi wa data binafsi.

Kusimamia Haki za Binadamu

Wanadamu wanapaswa kuwa na mfumo wa usimamizi wenye maana na pia mamlaka ya kufanya maamuzi juu ya mifumo ya AI ili kuhakikisha uwajibikaji na uwiano wa kimaadili.

Uwazi na urahisi wa kuelezea

Mifumo ya AI inapaswa kueleweka ili watumiaji na wadau waweze kufahamu jinsi maamuzi yanavyofanywa.

Wajibu na Uwajibikaji

Wajibu wazi na Mifumo ya uwajibikaji lazima ianzishwe kwa kuunda mfumo wa AI, muundo wa AI, matumizi yake na matokeo.

Uelewa na Stadi za Kidijiti

Serikali na wadau wanapaswa kukuza uelewa na stadi za AI na ufahamu wa umma ili kuwawezesha kushiriki wakiwa wanaelewa masuala kuhusu AI na pia ili watumie mifumo ya kidijitali kwa kuwajibika.

Utawala Bora na Ushirikiano wa Wadau Mbalimbali

Uendeshaji wa AI na masuala ya kiutamaduni kuhusiana nayo unapaswa kuhusisha michakato jumuishi, shirikishi na kurekebisha muktadha wa kiteknolojia na wa jamii inayobadilika.

Tanzania yaingia Awamu ya Vitu Kiotomatiki

Na Mwandishi wa Regulator

Nyenzo muhimu ya uchumi wa kidijitali – teknolojia inayoweza vitu kuwasiliana mtandaoni (IoT) iko katika hatua tofauti za maendeleo na kuenea Tanzania na matumizi ya mashine zinazowasiliana zenyewe (M2M) yanazidi kuongezeka.

IOT ni mtandao wa vifaa halisi na vitu vingine vilivyo na vijenzi vya kielektroniki na programu vinavyoweza kukusanya na kubadilishana data vyenyewe bila

kuingiliwa na binadamu. Michakato yake ni otomatiki.

Teknolojia za M2M huwezesha vitu, vifaa au vitu kubadilishana taarifa na kufanya vitendo bila kuingiliwa na binadamu au kuingiliwa kidogo sana kwa kutumia mitandao ya mawasiliano iliyopo au inayobadilika.

Kwenye M2M, sensa ndani ya vifaa zinakusanya taarifa, kuzichambua na kuzituma wakati halisi ndani ya muda mfupi sana.

Takwimu za mawasiliano za Juni 2026 zinaonyesha kuwa laini za simu za mkononi za M2M ziliongezeka kwa asilimia 33 kati ya Machi 2024 na Juni 2026, kutoka 929,683 hadi 1,233,467.

Usajili na matumizi ya laini za simu kwa mawasiliano kati ya mashine (M2M) ndani ya miaka miwili

Mtoa Huduma	Airtel	Halotel	TTCL	Yas	Vodacom	Jumla
Juni 2024	329,292	57,340	6,512	24,755	551,541	969,440
Juni 2025	350,749	78,687	4,501	61,370	588,048	1,083,355
Juni 2026	355,114	101,020	4,111	92,930	680,292	1,233,467
Ongezeko	25,822	43,680	2,401	68,175	128,751	264,027
Asilimia	7.8%	76%	(37%)	275%	23%	27%

Mawasiliano ya vitu kwa intaneti (IoT) na (M2M) ni viashirio muhimu vya mabadiliko ya kidijitali. Zinawezesha matumizi katika sekta muhimu kama vile kilimo, biashara, huduma za afya, usafiri na upangaji wa shughuli za usafiri na usafirishaji, nishati, shughuli viwandani, ufuatiliaji wa mazingira, huduma kwenye majiji ya kisasa huduma za dharura.

Katika kilimo, vifaa vya IOT vinaweza kufuatilia hali ya udongo, mifumo ya hali ya hewa, na ukuaji wa mazao. Vihisi vinaweza kupima kiwango cha unyevu wa udongo na kuwezesha kutoka kiasi cha maji kinachohitajika, hivyo kuwezesha umwagiliaji.

Vifaa vya huduma ya afya vya IOT vinaweza kufungwa mahali au kuvaliwa ili kufuatilia shughuli za kimwili, kunasa ishara muhimu na kurekodi vipimo vingine.

Vifaa hivi zinakusanya taarifa kwa wakati halisi, kuchambua na kuihamisha data kwa simu mahiri, kompyuta au wataalamu husika.

Viwanda hutumia vifaa vya IOT kusimamia shughuli na mipangilio ya uzalishaji. Vinafuatilia namna mashine zinavyofanya kazi, hugundua hitilafu, na kuboresha uzalishaji. Vinaweza

pia kufuatilia hali ya mazingira yanayohitajika kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa maalum ili kukidhi matakwa ya kisheria na kikanuni.

Maduka huzitumia teknolojia hizi kufuatilia mauzo, bidhaa ghalani na mwelekeo wa ununuzi.

Wasafirishaji hutumia vifaa vya IOT kudhibiti mienendo ya vyombo vyao. Hii ni pamoja na kufuatilia magari na kufuatilia utendaji wao, mienendo na matumizi ya mafuta.

Kwa kuunganisha vifaa na mifumo, IoT na M2M huongeza ufanisi, kuboresha utoaji wa huduma, na kuleta fursa mpya kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Usimamizi wa vifaa vya IoT na M2M unahitaji hatua kali za usalama ili kuzuia uduku. Ni muhimu sana kuwa na usimbaji fiche na udhibiti wa matumizi.

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imetenga nambari kuwezesha utoaji wa huduma za IoT na M2M. Aidha TCRA imeanzisha miongozo ya mawasiliano ya M2M. TCRA imeelezea taratibu na mahitaji ya huduma za mawasiliano ya M2M kupitia mitandao ya mawasiliano ya simu inayohitaji laini za simu na namba.



Mapya kwenye Sheria na Kanuni

Ada leseni za maudhui mtandaoni zapunguzwa, aina mpya yaanzishwa

Na Mwandishi wa Regulator

Aina mpya ya leseni ya huduma za maudhui mtandaoni imeanzishwa, ikiwa na masharti nafuu na msamaha wa ada mwaka mmoja.

Ada za leseni zimeshuka kati ya mara 10 na 20 kufuatia Marekebisho ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Mtandaoni ambayo yamenzisha leseni mpya kwa wanaoanza kutoa huduma.

Marekebisho hayo, yameondoa ada kwa wanaoanza kutoa huduma za vyombo vya habari mtandaoni kwa miezi 12. Baada ya hapo wanaweza kuomba leseni zinazodumu miaka mitatu na kufanya malipo stahiki.

Kanuni hizo mpya zilisainiwa na Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Paul Makonda Juni 27 mwaka huu na kuchapishwa kwenye gazeti la serikali tarehe 30 Juni.

Marekebisho hayo yanafanya idadi za leseni za huduma za maudhui mtandaoni kuwa tatu. Hizo ni za vyombo vya habari mtandaoni (televisheni, radio, majukwaa au blogu), watayarishaji maudhui na hii mpya kwa wanaoanza.

Leseni ya watayarishaji wa maudhui inamruhusu aliyepewa kukusanya maudhui kutoka vyanzo mbalimbali mtandaoni, ikiwa ni pamoja na kwenye tovuti, blogu na mitandao ya kijamii na kuyatoa kwa utaratibu rasmi kwa watoa huduma wengine au kupitia mfumo wa shitariki.

Waombaji wa leseni za vyombo vya habari mtandaoni kwa wanaoanza wanatakiwa kuwasilisha nyaraka mbili tu huku waombaji wa makundi mengine wakipaswa kuwasilisha sita.

Waombaji wa leseni za mtandaoni kundi la wanaoanza wanatakiwa kuwasilisha nyaraka mbili za lazima - nakala iliyothibitishwa ya kitambulisho chao cha taifa na cheti cha usajili wa jina la biashara - huku wale wa makundi mengine wakihitajiwa kuwasilisha sita.

Makampuni au mashirika yasiyo ya serikali yanatakiwa kuwasilisha nakala ya cheti cha kuanzishwa au cheti cha usajili wa jina la biashara, nakala ya hati ya mlipa kodi, nakala za vitambulisho vya taifa vya wanahisa au wanachama waanzilishi, orodha ya wamiliki na timu ya menejimenti.

Pamoja na hayo inawalazimu kuwasilisha wasifu wa wafanyakazi muhimu ambao watawajibika kuendesha kituo na ambao wanakidhi vigezo vya kuanzia vinavyohitajika kwa waandishi wa habari, pamoja na miongozo ya sera za uhariri kwa radio na televisheni mtandaoni.

Ada mpya kwa vyombo vya habari mtandaoni, huku za zamani zikiwa kwenye mabano ni shilingi 10,000 za maombi (100,000), ada ya awali, ada ya mwaka na ada ya

kuhuisha ya shilingi 50,000 (1,000,000).

Ada mpya ya maombi kwa watayarishaji maudhui mtandaoni ni shilingi 20,000 (100,000) na ada ya awali, ya mwaka na ya kuhuisha ni 100,000 (1,000,000).

Marekebisho ya kanuni na kuanzishwa kundi jipya la leseni za wanaoanza kutoa huduma za maudhui mtandaoni yanakusudia kuweka mazingira wezeshi ya uanzishwaji na usimamizi wa vyombo vya habari mtandaoni.

Kufikia 30 Juni mwaka huu kulikuwa na leseni za televisheni mtandao 210, radio mtandao 10, blogu za habari na matukio 66 na za watayarishaji maudhui mtandaoni tano (5).





Takwimu za Sekta ya Mawasiliano

Katavi yaongoza Upanuzi Miundombinu

Na Mwandishi wa Regulator

Katavi ni miongoni mwa mikoa mitano yenye kasi kubwa zaidi ya ujenzi wa minara na uwekaji vifaa ya mawasiliano ya simu ndani ya miaka miwili iliyopita, ripoti ya hali ya mawasiliano kufikia Juni 2026 imethibitisha.

Mkoa huo ulikuwa na ongezeko la wastani wa asilimia 47 ya minara ya mawasiliano na vituo vyenye vifaa vya teknolojia za kizazi cha nne na cha tano (4G na 5G) kati ya Juni 2024 na Juni mwaka huu.

Teknolojia hizo zinaitwa eNB kwa 4G na gNB kwa 5G, na huunganisha vifaa vya watumiaji na mitandao inayowezesha mawasiliano

ya kasi.


Teknolojia za 4G na 5G huwezesha upatikanaji wa intaneti na uhamishaji wa data kwa kasi ya juu sana na zinawezesha kupakia na kupakua video kwa ubora wa juu. Aidha, 5G inawezesha vifaa vingi vya watumiaji kuunganishwa bila kuathiri kasi na ubora wa huduma.

Mikoa mingine iliyokuwa na ongezeko la zaidi ya asilimia 20 katika usambazaji wa huduma za 4G na asilimia 50 kwa 5G mtawalia katika kipindi hicho ni Tabora, Pwani, Geita, Shinyanga, Lindi na Morogoro.

Mkoa wa Mjini Magharibi, Zanzibar uliongoza kwa

ongezeko kubwa zaidi la usambazaji wa huduma za 5G (asilimia 77.2 – kutoka vituo 232 hadi 411), ukifuatiwa na Simiyu (asilimia 70.5 – kutoka 193 hadi 329), Iringa (asilimia 58.4 – kutoka 291 hadi 461), Katavi (asilimia 57.1 – kutoka 126 hadi 198) na Dodoma (asilimia 56.1 – kutoka 326 hadi 506).

Nafasi ya jumla ya mkoa wa Katavi iliimarishwa na ongezeko la asilimia 42 katika usambazaji wa huduma za 4G – kutoka vituo 93 hadi 132.



Vifaa vya 5G kwenye minara viliongezeka kwa asilimia 159.7 kati ya Juni 2024 na Juni 2026. Teknolojia hii imeenea kwa asilimia 34.2 ya watu na asilimia 11.34 ya eneo la Tanzania.

Maelezo	Vifaa vya 5G vilivyofungwa kwenye minara	Kuenea huduma miongoni mwa watu	Kuenea huduma kijiografia
Juni 2024	754		Asilimia 2.2
Juni 2025	1,038	Asilimia 26	Asilimia 5.9
Juni 2026	1,958	Asilimia 34.18	Asilimia 11.34
Ongezeko	905	(ndani ya mwaka mmoja ni pointi 8.8)	Pointi 9.41
Asilimia ya ongezeko	159.7	(ndani ya mwaka mmoja ni asilimia 31.5)	Asilimia 415

Kuenea kwa Teknolojia ya 5G ndani ya miaka miwili

Kwa ujumla, minara mipya ya mawasiliano ya simu 1,382 ilijengwa kote Tanzania katika kipindi hicho, na kufanya jumla ya minara hiyo kufikia 9,933. Hili ni ongezeko la asilimia 16.2 kutoka minara 8,551 iliyokuwepo.

Vituo vyenye vifaa vya mawasiliano vilivyofungwa kwenye minara hiyo viliongezeka kwa asilimia 40.1, kutoka vituo 12,531 hadi 17,655.

Ongezeko hilo limechochewa na ujenzi wa minara mipya ya mawasiliano ya


simu na kuiongezea mingine uwezo wa kutoa huduma kupitia teknolojia za kisasa za mawasiliano chini ya mradi uliozinduliwa mwezi Mei 2023.

Laini za simu zaenea kwa asilimia 167

Mitandao mitano ya mawasiliano ya simu Tanzania ilikuwa na jumla ya laini zinazotumika 116,850,926 mwishoni mwa Juni 2026 – ongezeko la asilimia 48.7 kutoka 78,588,006 Juni 2024 na ongezeko la asilimia 4.51 kutoka 111,900,000 Machi mwaka huu


Kiwango cha kuenea miongoni mwa watu sasa kimefikia asilimia 167 kutokana na wateja kumiliki laini za simu zaidi ya moja kwa matumizi mbalimbali.

Laini zinazoweza mawasiliano kati ya mashine na mashine (M2M) ziliongezeka kwa asilimia 28, kati ya Juni 2024 na Juni mwaka huu – kutoka 962,928 hadi 1,233,467. Ziliongezeka kwa asilimia 4.3 kuanzia Machi mwaka huu, kutoka 1,182,797 hadi hizo 1,233,467..



Simu Janja

Simu janja zilienea kwa watu kwa asilimia 44.74 kufikia Juni 2026, kutoka asilimia 31.55 Juni 2024 na asilimia 42.5 Machi 2026.



Matumizi Intaneti, Data

Laini zilizotumika kupata huduma za intaneti ziliongezeka kwa asilimia 59.7, kati ya Juni 2024 na Juni 2026 – kutoka 39,311,477 hadi 62,793,986. Ziliongezeka kwa asilimia 6.48 kutoka laini 58,974,820 mwezi Machi 2026.



Laini zilizopata huduma ya Intaneti

Matumizi Data

Matumizi ya data yaliongezeka kwa asilimia 11.69 kutoka petabaiti 932 Machi 2026 hadi petabaiti 1,041 Juni mwaka huu. Matumizi haya yaliongezeka kwa asilimia 144.4 kati ya Juni 2024 na Juni mwaka huu, kutoka petabaiti 426 Juni 2024 hadi hizi za Juni mwaka huu.



Petabaiti ni kipimo cha ukubwa wa data kwenye kompyuta na vifaa vya kieletroniki vyenye sifa ya kompyuta.

Hata hivyo, pamoja na ongezeko hilo, watumiaji intaneti wanatumia asilimia 15.4 tu ya uwezo uliopo wa kuunganisha huduma ya intaneti kimataifa.

Uwezo uliopo, kwa kipimo cha gigabaiti kwa sekunde (Gbps) ni 17,690. Kinachotumika ni 2,731

Akaunti za pesa kwa simu

Mfumo thabiti na salama wa malipo ni mojawapo ya nguzo za uchumi wa kidijiti unaojengwa nchini. Tanzania inazidi kuendeleza mfumo jumuishi wa kifedha kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wanaoifanya miamala kupitia simu za mkononi.

Asilimia 74.5 ya laini za simu za mkononi zinazotumika zina akaunti za huduma za pesa kwa njia ya simu.

Akaunti za fedha kwa simu ziliongezeka kwa asilimia 7.5 kati ya Machi na Juni mwaka huu, kutoka 80,977,268 hadi 87,046,089


Kiashiria	Machi 2026	Juni 2026	Ongezeko	Kiwango cha Ukuaji (%)
Akaunti Hai	Millioni 80.98	Millioni 87.05	Millioni +6.07	+7.50%

Kombe la Dunia lasukuma mahitaji ving'amuzi

Hali iliyokuwepo ya kupungua kwa idadi ya ving'amuzi kwa matangazo ya televisheni imeondoka kutokana na kuanza kuongezeka kwa vifaa hivyo.

Idadi ya dekoda iliongezeka kutoka milioni 2.09 Machi 2026 hadi milioni 2.26 Juni 2026. Hapo awali, kulikuwa na mwelekeo wa kushuka ambapo idadi hiyo ilipungua kutoka milioni 2.3 Septemba 2025 hadi milioni 2.09 mwezi Machi.

Ongezeko hilo linatokana na hamu ya mashabiki wa mpira kufuatilia mashindano ya Kombe la Dunia la soka mwaka 2026 yaliyofanyika kuanzia tarehe 11 Juni hadi 19 Julai.




Matukio Ulaghai Mtandaoni

Matukio ya ulaghai na utapeli kupitia simu za mkononi yaliyoripotiwa yamepungua lakini bado ni tatizo sugu mikoani Rukwa na Morogoro.

Matukio yalipungua kwa asilimia 25.29, kutoka 9,816 katika robo iliyoishia Machi 2026 hadi 7,334 Juni 2026. Mikoa ya Rukwa na Morogoro bado inaongoza kwa matukio hayo, ikiwa na 2,495 na 2,199 mtawalia.

Hata hivyo, tatizo hilo limepungua kwa asilimia 69 kati ya Septemba 2023 na Juni mwaka huu, kutoka 23,328 hadi 7,334. TCRA imeendelea kutoa elimu kwa umma na watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu usalama wa mitandao. Katika elimu hiyo, TCRA inasisitiza umuhimu wa watumiaji kuwa waangalifu na jinsi ya kujilinda wanapokuwa mitandaoni ili kuepuka utapeli na wizi.



Kupanda na kushuka Huduma za Posta



Huduma za kuchukua na kusafirisha vifurushi zinaendelea kushika kasi nchini Tanzania, zikisaidiwa na mfumo wa Anwani za Makazi na Postikodi.

Huduma za Posta zilionyesha hali tofauti robo ya Aprili-Juni 2026, takwimu zikionyesha kupanda na kushuka kwenye maeneo mbalimbali.

Kulikuwa na ongezeko la vitu vilivyotumwa na kupokelewa kimataifa na kupungua kwa huduma hizo ndani ya nchi.

Vitu vilivyotumwa kwenda nje ya nchi viliongezeka kwa asilimia 40.8, kutoka 32,565 katika robo iliyoishia Machi 2026 hadi 45,850 mwezi Juni.

Vitu vilivyopokelewa kutoka nje viliongezeka kwa asilimia 52.2, kutoka 44,555 Machi 2026 hadi 67,800 Juni.

Vitu vilivyotumwa ndani ya nchi vilipungua kwa asilimia 9.9, kutoka 546,644 Machi 2026 hadi 492,335 Juni 2026. Vifurushi na barua vilivyopokelewa ndani ya nchi vilipungua kwa asilimia 1.6, kutoka 907,759 Machi hadi 893,673.

Mwelekeo mpya huduma za posta na usafirishaji vifurushi

TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za Posta na usafirishaji vifurushi. Hadi

kufikia Juni 2026 kulikuwa na watoa huduma 143 wakiwemo wasafirishaji kimataifa, ndani ya Tanzania, mijini na kati ya miji.

Kiujumla usafirishaji wa vifurushi umeongezeka kutokana na huduma zinazotolewa hasa na wenye leseni za usafirishaji ndani ya nchi, kupitia vyombo vya usafiri.